



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO
YA AMALI**

MHE. LELA MUHAMED MUSSA (MBM)

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA
KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

Mei, 2022

YALIYOMO

UTANGULIZI.....	1
MIRADI YA SEKTA YA ELIMU	4
UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2020/21	5
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI.	6
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	10
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU	14
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu.....	14
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti.....	16
Huduma ya Sayansi na Teknolojia.....	17
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	19
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	20
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI	22
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali.....	22
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima	25
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU	28
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia.....	28
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	29
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu.....	31
Huduma za Maktaba.....	33
Huduma ya Urajisi wa Elimu.....	35
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu.....	38
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	40
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli.....	42
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	44
Programu ndogo ya Uongozi Kujumla.....	44

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	47
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Elimu Pemba	50
MAPATO.....	51
MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2019/20 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU.....	51
Vipaumbele vya Wizara.....	52
MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU.....	54
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI.....	55
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	56
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU	57
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu.....	57
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti.....	57
Huduma ya Sayansi na Teknolojia.....	58
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	59
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	59
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI.....	60
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali.....	60
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.....	61
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU.....	62
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia.....	62
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	62
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu.....	63
Huduma za Maktaba.....	64
Huduma ya Urajisi wa Elimu.....	64
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	65
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu.....	66

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli.....	66
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	67
Programu ndogo ya Uongozi Kujumla.....	67
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti.....	68
Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba.....	69
MAKADIRIO YA MAPATO	70
JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI	70
SHUKURANI	71
KIAMBATISHO	73

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2022/2023.
- 2. Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana tena katika vikao vya baraza tukiwa wazima na afya njema. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kumaliza mfunzo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikukuu ya Eid El Fitr kwa salama na amani na leo hii tukaweza kukutana katika kikao hiki kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Namuomba Mwenyezi Mungu sasa aniwezeshe kuwasilisha hotuba hii kwa ufasaha mkubwa na pia awajaalie wasaa wajumbe wote wa baraza lako hili kuichangia vizuri na hatimae waweze kuipitisha kwa kauli moja.
- 3. Mheshimiwa Spika,** Nichukue nafasi hii kwa mara nyingine kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa

kuendelea kuniamini na kunikabidhi uongozi wa Wizara hii yenye mchango mkubwa katika kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali katika kuliletea taifa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pia, nimpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa nia yake safi ya kuliletea taifa hili maendeleo kwani katika kipindi cha muda mfupi tu wananchi wameanza kuona mabadiliko makubwa katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu. Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema, busara, hekima na umri mrefu wenye kheri naye ili aendelee kutuongoza vizuri. Pia, napenda kutoa pongezi zetu na shukurani za dhati kwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuwa karibu katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kufikia malengo ya Serikali.

- 4. Mheshimiwa Spika,** Pongezi za dhati zimfikie Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuiletea nchi hii maendeleo na kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kupitia sekta ya utalii kwa kuandaa filamu maalum “Royal Tour”. Jitihada hii inamanufaa makubwa kwa nchi yetu kwani itaongeza mapato ya nchi na kuweza kutatua changamoto zinazoikabili nchi yetu zikiwemo za elimu.

5. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii pia kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili kwa ufanisi mkubwa na kusimamia mijadala na hoja za wajumbe katika kuchangia utekelezaji wa vipaumbele vya mipango ya Serikali vyenye tija kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni busara, hekima, umahiri na uadilifu katika kutuongoza na kutekeleza majukumu yenu kwa maslahi ya wananchi wote na taifa kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika**, Shukurani za dhati nizifikishe kwa wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Kamati ya Bajeti chini ya uongozi mahiri wa Wenyeviti wake Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo kwa ushauri na maelekezo wanayotupatia katika kuimarisha sekta hii ya elimu. Aidha, niwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu kwa umakini wao na michango yao wanayoitoa kwa maendeleo ya nchi yetu.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Abdulgullam Hussein kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kutekeleza majumuku ya Wizara hii. Pia niwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakiwemo Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba, Wakurugenzi, wakuu wa vitengo, Wajumbe wa Bodi mbali mbali za Elimu,

Maafisa wa ngazi mbalimbali, bila kuzisahau Kamati zetu za skuli kwa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya elimu. Aidha, shukurani ziwafikie walimu, wazazi, wanafunzi na washirika wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa ushiriki na michango yao katika kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo huo wa imani na upendo kwa nchi yetu.

8. **Mheshimiwa Spika**, Mwisho nawashukuru sana watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao ambao umechangia katika kuimarisha huduma za elimu katika mwaka 2021/22. Nimatumaini yetu kuwa ushirikiano huo utaimarika zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za elimu.
9. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mpango wa elimu kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mashirikiano yaliyojengeka kwa muda mrefu kati ya Serikali, Wananchi na Wahisani wa ndani na nje katika kuchangia utekelezaji wa miradi mbali mbali.

MIRADI YA SEKTA YA ELIMU

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilitekeleza miradi mikuu mitano kama ifuatayo: -
 1. Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi
 2. Uimarishaji wa Elimu ya Msingi
 3. Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
 4. Uimarishaji wa Elimu ya Amali
 5. Uimarishaji Miundombinu ya Elimu

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA, 2021/22

- 11. Mheshimiwa Spika,** sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 wenye muundo wa programu sita. Programu hizi zimezingatia malengo ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Mpango Mkuu wa Elimu (ZEDP), Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Programu za Mpango wa Sekta ya Elimu ni kama ifuatavyo: -

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya 2: Elimu ya Sekondari

Programu ya 3: Elimu ya Juu

Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya 5: Ubora wa Elimu

Programu ya 6: Uongozi na Utawala

- 12. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa fedha wa 2021/2022, Programu hizi zote zilitengewa jumla ya TSh. 265,549,743,000/- zikiwemo TSh. 227,861,688,000/- kutoka SMZ na TSh. 37,688,055,000/- kutoka kwa wahisani. Kati ya fedha za SMZ, TSh. 182,278,300,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida zikiwemo TSh. 131,184,500,000/- za malipo ya mishahara na TSh. 45,583,388,000/- kwa miradi ya maendeleo. Fedha za wahisani zinajumuisha TSh. 14,568,055,000/- za ruzuku

kutoka Global Partnership for Education (GPE), KOICA, UNICEF, UNESCO, Milele Zanzibar Foundation, Table for Two (TfT) na Good Neighbors, na TSh. 23,120,000,000/- ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Benki ya Dunia.

13. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 167,880,285,165/- sawa na asilimia 58 ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, TSh. 118,990,574,888/- za matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 65.2 zilipatikana, kati ya hizo TSh. 97,791,271,699/- zilitumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na TSh. 21,199,303,189/- kwa kazi za utendaji. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya TSh. 48,889,710,277/- zilipatikana. Kati ya fedha hizo, TSh. 3,233,237,554/- sawa na asilimia 7.0 ni mchango wa Serikali na TSh. 45,666,472,723/- sawa na asilimia 121 ni kutoka kwa wahisani. Jadweli Nam. 10(a) na 10(b) yanatoa ufafanuzi zaidi.

14. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji halisi wa kila Programu ni kama ifuatavyo: -

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

15. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inahusisha uimarishaji na utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne na kumi na mbili.

16. Mheshimiwa Spika, Programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 79,037,993,000/-. Kati ya fedha hizo TSh. 57,312,685,000/- ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo TSh. 49,344,000,000/- za Mishahara ya wafanyakazi na TSh. 21,725,308,000/- kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2022, jumla ya TSh. 57,532,456,655/- sawa na asilimia 73 zilipatikana. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i. Jumla ya wanafunzi 15,357 wa Skuli 27 za Msingi zilizomo katika Mradi wa lishe wanaendelea kupatiwa chakula katika Wilaya Saba za Unguja na Pemba zikiwemo Wilaya ya Kaskazini A, Kaskazini B, Kati, Kusini, Micheweni, Wete, na Mkoani.
- ii. Serikali imerejesha darasa la saba katika ngazi ya elimu ya msingi, na hivyo elimu ya msingi sasa itakuwa ni ya miaka 7 kuanzia umri wa miaka 6.
- iii. Jumla ya washiriki 2,840 (Unguja 1820 na Pemba 1020) walihudhuria mafunzo juu ya kuwasaidia wanafunzi katika maendeleo yao ya elimu kupitia umoja wa mashirikiano ya Wazazi, Walimu na Jamii (UWAWAJA). Mafunzo hayo yalijumuisha wenyeviti wa kamati, wazazi, walimu wa madarasa ya maandalizi, walimu wa skuli za jamii na vituo vya TuTu pamoja na walimu wakuu katika skuli zenye madarasa ya maandalizi Unguja na Pemba.
- iv. Jumla ya walimu 2,436 wa madarasa ya maandalizi na vituo vya TuTu wamejengewa uwezo wa kutumia

hadithi kama mbinu ya kumsaidia mtoto kuweza Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa urahisi na kwa haraka.

- v. Jumla ya vituo 50 vya TuTu Unguja na Pemba vimepatiwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo, penseli manila sheets markerpen, gundi, sahani za karatasi, karatasi za A4 nyeupe na za rangi.
- vi. Ujenzi wa Skuli nne za maandalizi umekamilika pamoja na kupatiwa samani katika maeneo ya Donge Chechele, Mwera Gudini kwa Unguja na Kifundi na Kipapo kwa Pemba. Aidha, kupitia mradi wa UVIKO 19, Serikali inaendelea na ujenzi wa Skuli 22 mpya za maandalizi na Madarasa 105 ya maandalizi yakiwemo madarasa 47 mapya na madarasa 58 ya kukamilisha yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi Unguja na Pemba.
- vii. Ujenzi wa madarasa 61 ya msingi yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi umekamilika, yakiwemo madarasa 38 Unguja na madarasa 23 Pemba.
- viii. Serikali kupitia Mradi wa UVIKO 19, inaendelea na ujenzi wa madarasa 589 ya skuli za msingi yakiwemo madarasa 335 Mapya na madarasa 254 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, kupitia mradi huo, Serikali inajenga skuli saba za msingi katika maeneo ya Kidongochekundu, kwabitihamrani, Mwanakwerekwe, Jendele, Kwale, Mwambe na Pujini. Skuli ya Jendele Unguja na Skuli ya Pujini Pemba zitakuwa ni za elimu mjumuisho ambazo wanafunzi

wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji maalum watasoma pamoja.

- ix. Ujenzi wa vyoo 80 umekamilika katika skuli za Kandwi, Ubago na Kikungwi kwa Unguja na Skuli za Kisiwapanza, Mwambe na Tumbe kwa Pemba. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa vyoo 1,396 kwa Unguja na Pemba vikiwemo vyoo 525 vya maandalizi na 871 vya msingi kupitia mradi wa UVIKO 19.
- x. Jumla ya madarasa 31 na ofisi 4 yamefanyiwa ukarabati Unguja na Pemba katika skuli za Chukwani, Kiembesamaki, Jang'ombe, Jumbi Msingi, Ghana, Ubago na Shaurimoyo.
- xi. Ziara za ufuatiliaji katika skuli 234 za Maandalizi na Msingi, Unguja 140 na Pemba 94, zenye lengo la kuimarisha utendaji kazi zimefanyika. Miongoni mwa mambo yaliyofuatiliwa ni uwajibikaji wa walimu katika usomeshaji, mazingira ya usafi na suala la udhalilishaji.

Matokeo ya Muda Mfupi;

- i. Jumla ya wanafunzi 95,613 sawa na asilimia 81.0 wameandikishwa katika madarasa ya maandalizi kwa mwaka 2022.
- ii. Jumla ya wanafunzi 52,038 wapya wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2022. Kati yao 26,671 ni wanaume na 25,367 ni wanawake. Kati ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza, wanafunzi 43,194 sawa na asilimia 83.0 wamepitia

elimu ya maandalizi. Uandikishaji unafanya idadi ya wanafunzi wote katika ngazi hii ya msingi kwa mwaka 2022 kufikia 360,330 sawa na asilimia 98.0 Jadweli Nam. 14 linatoa ufafanuzi zaidi.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.

17. Mheshimiwa Spika, Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya sekondari. Jumla ya TSh. 110,014,054,000/- zilipangwa kutumika, kati ya fedha hizo TSh. 58,840,132,000/- ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo TSh. 51,351,468,000/- za mishahara ya wafanyakazi na TSh. 51,173,922,000/- kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2022, jumla ya TSh. 74,899,923,979/- zilipatikana sawa na asilimia 56. Utekelezaji kwa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya mitihani ya Taifa kwa skuli za sekondari zenye Kidato cha Nne na cha Sita vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli hizo. Aidha, vifaa kwa somo la uchoraji (Fine Arts), masomo ya maarifa ya nyumbani (home economics), na somo la Kompyuta kwa skuli nne (Ben-Bella, Aboud Jumbe, Forodhani na Mwanakwerekwe "C") navyo vimenunuliwa kwa mahitaji ya mitihani ya Kidato cha Nne 2021. Aidha, Jumla ya madaftari 1,560,036 yamenunuliwa na kupatiwa wanafunzi.
- ii. Jumla ya Vitabu 67,000 vya somo la Kiingereza kwa Kidato cha Kwanza na cha Pili vimenunuliwa kutoka

Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) na kusambazwa kwa wanafunzi.

- iii. Jumla ya TSh. 2,452,600,000/= zimetumika kulipia deni la gharama za mitihani ya wanafunzi wa Kidato cha Nne kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2019 hadi 2021. Deni hilo sasa limebakia TZS 100,000,000/- .
- iv. Wizara imeendelea kuwapatia huduma ya chakula wanafunzi 2,263 wanaoishi dahalia. Dahalia hizo ni Mazizini, Hasnuu Makame, Donge na Mikunguni kwa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Fidel Castro, CCK Kiuyu, Chasasa, Utaani, Mohamed Pindua na Kengeja ufundi.
- v. Jumla ya wanafunzi 213 wamefaulu kujiunga na Vipawa katika skuli ya Sekondari ya Lumumba na Fidel castro na wanafunzi 2,167 wamefaulu kujiunga na Michepuo mbalimbali kutoka skuli za Serikali na Binafsi, Unguja na Pemba.
- vi. Jumla ya wanafunzi 15,677 wamefaulu mtihani wa Kidato cha Nne uliofanyika Novemba, 2021 na wanafunzi 4,411 wataendelea na masomo ya Kidato cha Tano katika skuli mbalimbali za Serikali Unguja na Pemba. Aidha jumla ya wanafunzi 11,320 wataendelea kusoma fani mbalimbali kwa ngazi ya stashahada.
- vii. Jumla ya wanafunzi 3,373 (wanaume 1,728 na wanawake 1,645) wanatarajiwa kufanya mtihani wa kumalizia kidato cha sita kuanzia tarehe 09/05/2022 hadi tarehe 27/05/2022.

- viii. Ukarabati mkubwa wa skuli ya Paje Mtule na Chwaka Tumbe umekamilika na ukarabati wa skuli ya Haile Selassie unaendelea. Aidha, ukarabati wa skuli 24 Unguja na Pemba na ujenzi wa vyoo 297, kupitia mradi wa UVIKO 19 umeanza na uko katika hatua mbalimbali.
- ix. Jumla ya madarasa 35 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi yamekamilika katika skuli za Nungwi, Tunguu, Mtoni Kigomeni, Mahonda, Kidoti, Gando na Micheweni. Aidha, jumla ya madarasa 130 na ujenzi wa skuli nne katika maeneo ya Mtopepo, Bweleo, Makangale na Pujini unaendelea.
- x. Taratibu za ujenzi wa skuli tatu za Sekondari za kisasa zenye dahalia katika Mikoa ya Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi na Kaskazini Pemba zinaendelea. Michoro ya skuli hizo zote tatu imekamilika. Wizara imetangaza zabuni kwa wakandarasi kwa ajili ya kuipata kampuni ya ujenzi.
- xi. Ujenzi wa maabara kwa lengo la kuimarisha Elimu ya sayansi umeanza katika skuli 10 za Sekondari za Fukuchani, Tumbatu, Chukwani, Fujoni, Machui Jendele kwa Unguja na kwa Pemba Skuli za Uondwe, Chanjamjawiri, Chambani na Wambaa.
- xii. Jumla ya maabara za skuli 85 za Pemba zimefanyiwa uhakiki wa kutambua kemikali zilizopitwa na wakati ili kuweza kuziangamiza. Aidha, walimu 85 kutoka katika skuli hizo wamejengewa uwezo wa jinsi ya kuzihifadhi na namna ya kuziangamiza kemikali zilizopitwa na

muda.

- xiii. Taratibu za ujenzi wa dahalia ya wanawake katika skuli ya Paje Mtule, Chwaka Tumbe na Lumumba zinaendelea ambapo Wizara tayari imesaini hati ya makubaliano na wahisani wa Korea kwa ajili ya ujenzi wa dahalia katika skuli hizo.
- xiv. Kufuatia ajali ya moto katika dahalia ya Skuli ya Utaani na Chasasa Pemba iliyotokea siku ya tarehe 8/03/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewafariji wanafunzi wote waliokuwa wakiishi dahalia hiyo na walimu wa skuli hizo kwa kuwapatia misaada mbalimbali ikiwemo chakula, magodoro na fedha taslim.
- xv. Jumla ya seti za vikaliyo 11,442 za wanafunzi wa ngazi ya elimu ya sekondari zimesambazwa katika Skuli za Sekondari Unguja na Pemba (5,442 Unguja na 6,000 Pemba).
- xvi. Wizara imezizawadia fedha taslim TZS 347,037,338/- skuli 97 za Sekondari Unguja (56) na Pemba (41) zilizofanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa ya Kidato cha Pili na cha Nne.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya wanafunzi 111,147 kati yao wanaume 49,465 na wanawake 61,682 wameandikishwa katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ya awali (kidato 1 – 4). Jadweli Nam. 16 linatoa ufafanuzi zaidi

- ii. Jumla ya wanafunzi 6,612 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya Sekondari ya juu (kidato 5-6) wakiwemo wanaume 3,282 na wanawake 3,330. Jadwali Nam.21(a) linatoa ufafanuzi zaidi.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

18. **Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya programu ya Elimu ya Juu ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujijajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia; Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

19. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ndogo ilitengewa jumla ya TSh. 1,115,837,000/- za SMZ kwa kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Cheti na Stashahada na kutoa mafunzo ya walimu kazini. Kati ya fedha hizo TSh. 444,705,000/- zilitengwa kwa utoaji wa mafunzo na utendaji wa kazi mbalimbali za ofisi na TSh. 671,132,000/- ni kwa ajili ya malipo ya mshahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2022, jumla ya TSh. 701,927,525/- sawa na asilimia 63 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -
 - i. Jumla ya walimu 303 wa skuli za msingi (darasa la 5 na 6) na walimu 1619 wa sekondari (FI - II) wamepatiwa

mafunzo juu ya mbinu za ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji na kuinua kiwango cha ufaulu.

- ii. Jumla ya Wakufunzi 100 wa Vyuo vya Kiislamu Unguja na Pemba na walimu 33 wa Skuli za Sekondari wamepatiwa mafunzo kuhusiana na mbinu za umahiri za ufundishaji.
- iii. Mafunzo kwa Waratibu wa Vituo vya Walimu na Washauri wa Masomo 33 juu ya mbinu sahihi za utungaji mitihani, utayarishaji na uandishi wa ripoti yametolewa.
- iv. Uandikishaji wa wanafunzi kwa upande wa Vyuo vya Ualimu (CCK) Unguja na Pemba umefanyika. Jumla ya wanafunzi 1,500 (Unguja 900 na Pemba 600) wamefanya usaili wa kujiunga na Vyuo hivyo na wanatarajiwa kuanza masomo Julai, 2022.

Matokeo ya muda mfupi

Jumla ya wanafunzi 1,549 wanasomea mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya Astashahada na shahada ya Ualimu. Kati yao, wanafunzi 1,140 wakiwemo wanaume 130 na wanawake 1,010 wanasomea Ualimu katika Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja na wanafunzi 409 wakiwemo wanaume 130 na wanawake 279 katika Chuo cha Kiislamu Kiuyu Pemba.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

- 20. Mheshimiwa Spika,** Lengo la huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ni kuimarisha maandalizi katika fani za kitaaluma na ajira. Jumla ya vyuo vitatu vinahusika na utoaji wa huduma hii vikiwemo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait na Chuo Kikuu cha Zanzibar.
- 21. Mheshimiwa Spika,** Uandikishaji katika vyuo hivyo umefikia wanafunzi 9,370 wakiwemo wanaume 3,889 na wanawake 5,481. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa mwaka 2021/2022 kilitengewa ruzuku ya TSh. 15,689,000,000/- . Kati ya fedha hizo TSh. 1,387,200,000/- zilitengwa kwa matumizi ya kawaida na TSh. 14,301,800,000/- kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 10,484,540,180/- sawa na asilimia 67 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -
- i) Wafanyakazi 100 wanalipiwa gharama za masomo ya muda mrefu katika kada za taaluma na uendeshaji. Kati ya wafanyakazi hao 47 wa ngazi ya Uzamivu, 37 ngazi ya Uzamili, 15 shahada ya kwanza na mmoja ngazi ya Astashahada.
 - ii) Jumla ya wanafunzi wapya 2,532 wakiwemo wanaume 1,069 na wanawake 1,463 wamedahiliwa kujiunga na chuo kwa muhula wa kwanza
 - iii) Chuo kupitia taasisi ya Utalii Maruhubi kimefanya mapitio ya mtaala wa kozi zote za ukarimu kwa ngazi ya cheti (NTA Level 4).

- iv) Chuo kimeshiriki katika kongamano la Kiswahili la BAKIZA ambapo wanafunzi 10 walishiriki.
- v) Vifaa mbali mbali vya skuli ya meno vimenunuliwa vikiwemo viti 5 vya kung'olea meno, "compressor" 3, majiko matatu ya kupikia vifaa (autoclave) na phantom 5 za kufundishia.

Matokeo ya muda Mfupi

- i) Jumla ya wanafunzi 5,903 wamedahiliwa katika ngazi mbali mbali. Kati yao wanaume ni 2,490 na wanawake 3,413.
- ii) Jumla ya wanafunzi 1,896 wamehitimu katika ngazi za Shahada ya uzamili, shahada ya kwanza, stashahada na astashahada katika programu mbali mbali na kutunikiwa vyeti.

Huduma ya Sayansi na Teknolojia

- 22. Mheshimiwa Spika**, huduma ya Sayansi na Teknolojia ina umuhimu mkubwa katika kuinua kiwango cha elimu ya Sayansi na Teknolojia na kuimarisha uchumi wa nchi. Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ndio inayohusika kwa kiasi kikubwa katika kutoa huduma hii. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Taasisi ilitengewa ruzuku ya TSh. 2,008,900,000/- . Kati ya fedha hizo, TSh. 485,300,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 1,523,600,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 1,240,456,816/= sawa na asilimia 62 zilipatikana. Fedha hizi zilitumika katika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i. Kukamilika ujenzi wa jengo la hanga, ambalo litapunguza tatizo la kufanya mazoezi ya vitendo katika Kiwanja cha ndege cha Abeid A. Karume na kuongeza fursa kwa wanafunzi katika kujifunza.
- ii. Kusajili wanafunzi wapya 886, wanaume 784 na wanawake 102 kwa fani zote za Taasisi, shahada ya kwanza 152 (38 w'ke), Stashada 205 (51 w'ke) na ngazi ya cheti ni 529 (13 w'ke).
- iii. Jumla ya watumishi tisa walijajiriwa katika Taasisi, kati yao wanne wa kada ya ukufunzi na watano kada za uendeshaji kwa njia ya Uhamisho kutoka Wizara ya Elimu pamoja na Utumishi wa Umma.
- iv. Kuendeleza mafunzo mapya ya shahada ya kwanza ya uhandisi umeme na uhandisi majenzi na kuiendeleza zaidi Taasisi na kuisaidia jamii kwa kutumia Sayansi na Teknolojia
- v. Kukamilisha uandishi wa mitaala ya mafunzo mapya ya usarifu wa mazao ya baharini, mbogamboga na matunda, “digital development technology” na wood technology katika ngazi ya stashahada. Pia somo la Telecommunication and Network Techonogy Engineering katika ngazi ya Shahada ya kwanza.

Matokeo ya muda Mfupi

Jumla ya wanafunzi 1,562 wakiwemo wanawake 238 na wanaume 1,324 wanaendelea na masomo katika fani mbalimabli zikiwemo, Shahada ya kwanza ya uhandisi wa

matengenezo ya ndege, uhandisi wa elektroniks na umeme na uhandisi ujenzi.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

23. Mheshimiwa Spika, Mikopo kwa ajili ya wanafunzi wanaojiunga na kuendelea na masomo katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu, ndani na nje ya nchi inatolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Bodi ilitengewa jumla ya TSh. 11,646,400,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 11,271,000,000/- ni kwa ajili ya utoaji wa mikopo na ufuatiliaji na TSh. 375,400,000/- ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 4,783,947,760/= sawa na asilimia 41 zilipatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i. Kutoa mikopo kwa wanafunzi 4,659 wa elimu ya juu wakiwemo wanafunzi wapya 1,526 na wanafunzi 3,133 wanaoendelea na masomo yao katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya Tanzania.
- ii. Jumla ya wanafunzi saba wamepatiwa nafasi za ufadhili wa masomo nje ya nchi zilizotolewa na washirika wa maendeleo wakiwemo Ras Al-Khaimah (3) na nafasi (4) kutoka Serikali ya Pakistan.
- iii. Jumla ya wanafunzi 187 wenye ufaulu wa ngazi ya juu wa matokeo ya Kidato cha Sita wakiwemo wapya 20 na wanaoendelea na masomo 167 wamepatiwa ufadhili wa masomo wa SMZ.
- iv. Jumla ya wanafunzi wapya 43 wamepatiwa ufadhili

wa masomo kwa vyuo vya ndani ya nchi wakiwemo 24 kupitia taasisi za Darul Imaan katika Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu na 19 kupitia Shirika la “Direct Aid” lililotoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait cha Chukwani.

- v. Jumla ya wanafunzi 1,284 wakiwemo wanafunzi 874 wanaosoma vyuo vya Zanzibar, 297 katika vyuo vya Tanzania Bara na 113 wa vyuo vya nje ya Tanzania wanatarajiwa kuhitimu masomo yao katika fani na ngazi mbalimbali za elimu ya juu.

Matokeo ya muda Mfupi

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 jumla ya TZS 3,200,000,000/- bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 77.8 ya lengo lililowekwa.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

- 24. **Mheshimiwa Spika**, huduma hii inatolewa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu na ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Kitengo kilitengewa jumla ya TSh. 50,000,000/= kutoka Serikalini. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 13,980,375/= sawa na asilimia 27.9 zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i. Ziara za ufuatiliaji na tathmini kwa Taasisi za Elimu ya Juu 16, kuangalia utoaji wa Elimu na uendeshaji

katika Taasisi hizo pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali za wanafunzi wanazokutana nazo Vyuoni zimefanyika.

- ii. Jumla ya taasisi 23 za elimu ya juu zilishiriki maonesho ya Wiki ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na Elimu ya Juu ili waweze kuchagua fani za Vyuo Vikuu zinazoendana na masomo yao.
- iii. Nafasi za masomo za kujiunga na elimu ya juu za ndani na nje ya nchi ya Tanzania zimetangazwa pamoja na kuweka kumbukumbu za wanaorudi kutoka masomoni. Nafasi zilizotangazwa ni kutoka nchi za Qatar, Misri katika Chuo Kikuu cha El – Just, Jumuiya ya Madola Russia, Hungary, China, Serbia, Australia, Turkey, Mauritius na Azerbaijan. Nafasi hizo zilijumuisha fani mbalimbali zikiwemo; Udaktari, Uchumi, Ukandarasi, Uwalimu, Uguzi na Sayansi ya Mazingira, Kilimo, Usimamizi wa Biashara na Utawala, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya tehamu kwa viwango vya Shahada ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu.
- iv. Jumla ya waombaji 145 (wanaume 96 na wanawake 49) waliwasilisha maombi yao na walionufaika kupata nafasi hizi ni wanafunzi 39 (wanaume 23 na wanawake 16).
- v. Ziara za ufuatiliaji na tathmini kwa Taasisi za Elimu ya Juu 16, kuangalia utoaji wa Elimu na uendeshaji katika Taasisi hizo pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali za wanafunzi wanazokutana

nazo Vyuoni zimefanyika.

- vi. Jumla ya taasisi 23 za elimu ya juu zilishiriki maonesho ya Wiki ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na Elimu ya Juu ili waweze kuchagua fani za Vyuo Vikuu zinazoendana na masomo yao.

Matokeo ya muda mfupi;

Jumla ya wanafunzi 20 waliripoti kutoka masomoni wakiwemo wanaume 8 na wanawake 12.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

25. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inalenga kuwajengea vijana uwezo katika ushindani wa soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo ya amali na mbadala. Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima.

Programu Ndogo ya Mafunzo ya Amali

26. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu hii ndogo ilitengewa jumla ya ruzuku ya TSh. 9,082,200,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 7,187,000,000/- ni kwa ajili ya utoaji wa mafunzo ya amali na TSh. 1,895,200,000/- ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 2,126,105,380/= kutoka SMZ zilipatikana sawa na asilimia 23. Utekelezaji halisi kwa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kupitia ZBC redio na Televisheni imeweza kutoa matangazo mbalimbaili kwa ajili ya usajili wa vijana katika vyuo vya Mfunzo ya Amali.
- ii. Mamlaka ya Mafunzo ya Mafunzo ya Amali imeratibu ufanyaji wa Mtihani wa Taifa wa Mamlaka ya Mafunzafunzo Amali kwa wanafunzi wa vituo 14 vikiwemo vinne vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na 10 vya binafsi ambapo jumla ya wanafunzi 2,353 walishiriki katika mitihani hiyo. Wanafunzi 1,563 (wanaume 950 na wanawake 612) sawa na asilimia 66 wamefaulu mitihani yao.
- iii. Jumla ya vituo saba vinavyotoa Mafunzo ya Amali (viwili Unguja na vitano Pemba) vimepatiwa Usajili vikiwemo Alnoor Training center, Capital Technology center, Center for Proffesional and Vocational Training, Samael Vocational Training Center, Stone Town Youth Center, Wete Vocational Training Center, na Zanzibar Center for Excelence in Tourism na Vituo vitatu vimerudia usajili baada ya usajili wa awali kumaliza muda wake vikiwemo ICPS Vocational Traning Center, Experience Vocational Training Centre na Zan. Vocational Training Centre
- iv. Jumla ya vituo 25 vinavyotoa Mafunzo ya Amali vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida kwa lengo la kutathmini kiwango cha mafunzo yanayotolewa. Miongoni mwa vyuo vilivyokaguliwa ni Fama Culture, Inlightment Training Center, Chuo cha Mafunzo ya

Amali Makunduchi, Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe na Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo.

- v. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imewatambua mafundi wazoefu ambao hawakupita katika mfumo rasmi wa mafunzo kwa kuwasajili na kuwaingiza katika kanzidata kwa hatua ya awali. Aidha, jumla ya vijana 222 wamefanyiwa mitihani wa fani ya ushoni, upishi, umeme, uchoraji na mapambo na elektroniki. Lengo ni kutathmini mapungufu walionayo katika fani ambazo wanauzoefu nazo ili kuwapatia mafunzo ya kurekebisha mapungufu yao na hatimae kuweza kurasimishwa kwa kupatiwa vyeti.
- vi. Rasimu ya muongozo wa urasimishaji wa mafundi wazoefu (RPL guideline) imetayarishwa na tayari imeshapitiwa na wadau Unguja na Pemba. Aidha, Rasimu ya awali ya muongozo wa vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali (Prospectus) imeanza kuandaliwa kwa lengo la kuwafanya vijana wanaojiunga na vyuo kuelewa utaratbu mzima wa kujiunga hadi kumaliza mafunzo katika vyuo hivyo.

Matokeo ya muda mfupi;

- i) Jumla ya vituo saba vinavyotoa Mafunzo ya Amali (viwili Unguja na vitano Pemba) vimepatiwa Usajili.
- ii) Jumla ya vijana 1,703 wapo katika vyuo hivyo kati ya hao 905 ni wapya waliosajiliwa katika vyuo vitano

vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa masomo 2022.

Programu Ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

27. Mheshimiwa Spika, Lengo kubwa la programu hii ni kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii. Utekelezaji wa programu hii unasimamiwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 7,266,030,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 6,220,667,000/- kwa ajili ya kazi za maendeleo kwa programu ya Mafunzo ya Amali na TSh. 1,045,360,000/- ni kwa ajili ya programu ya Elimu Mbadala na Watu Wazima ambazo TSh. 537,705,000/- ni za shughuli za utoaji wa elimu mbadala na elimu ya watu wazima na TSh. 507,655,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 507,235,475/- sawa na asilimia 48.5 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya madarasa ya kisomo 429 (193 Unguja na 236 Pemba) yenye wanakisomo 6,406 yanaendelea kutoa Elimu ya Kisomo cha Watu Wazima Unguja na Pemba.
- ii. Jumla ya wanakisomo 5,453 wa Kisomo cha Watu Wazima wamefanyiwa Upimaji katika hatua zote nne za kisomo. Aidha wanakisomo 370 wa hatua ya nne wamekombolewa kupitia upimaji huo.
- iii. Jumla ya walimu 50 wa madarasa ya kisomo

wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kufundisha watu wazima.

- iv. Jumla ya wanafunzi 3,350 (wanawake 752 na wanaume 2,598) wamesajiliwa kujiunga na madarasa ya Elimu Mbadala Unguja na Pemba. Kati yao 1,081 Unguja (wanawake 194 na wanaume 887), Pemba 2,269 (wanawake 558 na wanaume 1,711).
- v. Madarasa ya Elimu Mbadala yameongezeka kutoka 35 (Unguja 22 na Pemba 13) na kufikia 98 (Unguja ni 47 na Pemba 51) baada ya kuanza kwa Programu ya kuwarejesha watoto skuli.
- vi. Maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima yamefanyika. Uzinduzi na kilele vilifanyika Wilaya ya Micheweni katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.
- vii. Jumla ya vikundi 90 (49 Unguja 41 Pemba) vyenye jumla ya wanachama 1,755 (wakiwemo wanawake 1,639 na wanaume 116) vimeendelezwa kwa lengo la kuwapunguzia wanawake utegemezi na umasikini wa kipato.
- viii. Jumla ya wanafunzi 241 (wanaume 123 na wanawake 118) wamesajiliwa katika vituo vya kujiendeleza kwa Unguja na Pemba. Aidha, wanafunzi 74 (wanawake 70 na wanaume 4) walioshindwa kuendelea na masomo yao baada ya mthani wa Kidato cha Pili na cha Nne wameandikishwa katika Kituo cha Sayansi Kimu Forodhani kusomea fani ya Upishi, Ushoni, Kudarizi na Kufuma.

Matokeo ya muda mfupi;

- i) Jumla ya wanakisomo Waliomo madarasani ni 6,406 wakiwemo wanaume 766 na wanawake 5,640. Pemba wanakisomo 3,205 na Unguja wanakisomo 3,201.
- ii) Jumla ya wanafunzi 11,735 wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 waliokuwa nje ya skuli wamerejeshwa skuli chini ya programu ya kuwarejesha watoto skuli. Kati yao Unguja 5,073 (1,447 wanawake na 3,626 wanaume) na Pemba 6,662 (1,843 wanawake na 4,819 wanaume).
- iii) Jumla ya wanafunzi 401 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 wameandikishwa katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo Unguja na Kituo cha Wingwi Mtemani Pemba. Kati yao, wanaume 267 na wanawake 134. Vijana hawa wanasomea fani mbalimbali zikiwemo Umeme, Ushoni, Upishi, Udobi, Mafunzo ya Kompyuta, Uchoraji, kilimo na Ufugaji, Utunzaji Nyumba pamoja na masomo ya kawaida ili kuwajengea uwezo wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.
- iv) Jumla ya wanafunzi 4,565 wamefanya mtihani wa faragha wa Kidato cha Nne. Kati ya hao, wanafunzi 2,224 sawa na asilimia 48.72 ya watahiniwa wote wamefaulu. Aidha, wanafunzi 129 (wanaume 97 na wanawake 32) waliofanya mtihani wa faragha wa Kidato cha Sita Mei, 2021 kwa Unguja na Pemba ambao ni sawa na asilimia 74.42 wamefaulu.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

- 28. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kuhakikisha elimu itolewayo katika ngazi zote za elimu ni yenye ubora kwa manufaa ya mwenye kuhitimu, jamii na taifa kwa ujumla. Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo: -

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

- 29. Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya huduma hii ni kutayarisha mitaala ya elimu na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu. Taasisi ya Elimu ndiyo inayohusika na utekelezaji wa utoaji wa huduma hii. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya TSh. 738,400,000/, kati ya fedha hizo, TSh. 294,900,000/- ni kwa ajili ya matayarisho ya mitaala na TSh. 443,500,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2022, jumla ya TSh. 441,577,190/- sawa na asilimia 60 zilipatikana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo: -

- i. Jumla ya mihutasari 14 ya mtaala mpya wa 2019 wa Elimu ya Msingi imeandikwa ikiwemo 6 ya ngazi ya Msingi Awali (Darasa la I - III) na 8 ya Msingi Juu (Darasa la IV-VII). Aidha, Taasisi imetafsiri kwa lugha ya Kiingereza mihutasari yote ya elimu ya Maandalizi na Msingi kwa ajili ya matumizi katika skuli za binafsi na jamii.

- ii. Mihutasari ya darasa la saba imesambazwa na kuanza kutumika katika skuli zote za Msingi Unguja na Pemba.
- iii. Miongozo ya masomo kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia imeandikwa kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya msingi darasa la saba katika skuli za serikali na binafsi.
- iv. Rasimu ya muongozo wa vigezo vya kuandika vitabu imetayarishwa kwa madhumuni ya kudhibiti ubora wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi.

Matokeo ya Muda mfupi

- i) Jumla ya mihutasari 14 ya mtaala mpya wa 2019 wa Elimu ya Msingi imeandikwa
- ii) Mihutasari ya darasa la saba imesambazwa na kuanza kutumika katika skuli zote za Msingi Unguja na Pemba.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

- 30. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya TSh. 5,641,200,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 5,123,100,000/- ni kwa ajili ya kazi ya upimaji na TSh. 518,100,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 4,687,430,067/- sawa na asilimia 83 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma ya Upimaji na Tathmini ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya wanafunzi 50,952 (wanaume 26,080 na wanawake 24,872) wa Darasa la Nne waliandikishwa kufanya mtihani wa Darasa la Nne. Wanafunzi halisi waliofanya mtihani ni 48,248 (wanaume 24,127 na wanawake 24,119) sawa na asilimia 94.7 ya walioandikishwa.
- ii. Jumla ya wanafunzi 34,218 (wanaume 16,383 na wanawake 17,835) waliandikishwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi Darasa la Sita. Kati yao wanafunzi 33,010 (wanaume 15,528 na wanawake 17,482) sawa na asilimia 96.46 walifanya mtihani.
- iii. Jumla ya wanafunzi 33,792 (wanaume 15,445 na wanawake 18,347) waliandikishwa kufanya mtihani wa kumaliza Kidato cha Pili, ambapo wanafunzi 32,279 (Wanaume 14,543 na Wanawake 17,736) sawa na asilimia 95.52 walifanya mtihani.
- iv. Jumla ya wanafunzi 225 (wanaume 18 na wanawake 207) waliandikishwa kufanya mtihani ya Cheti cha Ualimu Maandalizi (ECD), ambapo wanafunzi wote 225 sawa na asilimia 100 wamefanya mtihani.
- v. Baraza la Mitihani limewaandikisha Walimu wanafunzi 202 wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kumaliza masomo ya Stashahada ya Ualimu kwa ngazi ya Msingi na Sekondari katika Vyuo vya Kiislamu vya Unguja na Pemba, kati yao 38 ni wanaume na 164 ni wanawake. Mitihani hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 03 – 11 Mwezi wa Mei, 2022.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa Darasa la Nne ni 39,273 sawa na asilimia 81.40, kati ya hao, wanaume ni 18,111 sawa na asilimia 37.54 na wanawake ni 21,162 sawa na asilimia 43.86 ya watahiniwa wote.
- ii. Wanafunzi waliofaulu mtihani wakumaliza Darasa la sita ni 32,462 sawa na asilimia 98.34, wanaume ni 17,376 sawa na asilimia 52.64 na wanawake ni 15,086 sawa na asilimia 45.70 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha, wanafunzi 1,363 wamefaulu kuendelea na masomo yao katika madarasa ya vipawa (174) na michepuo (1,189) sawa na asilimia 4.1.
- iii. Wanafunzi 25,393 sawa na asilimia 78.7 wamefaulu mtihani wa Kidato cha Pili na kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu wakiwemo wanaume 15,107 sawa na asilimia 46.8 na wanawake 10,286 sawa asilimia 31.87
- iv. Wanafunzi wote 225 sawa na asilimia 100 wamefaulu mtihani wa Cheti cha Ualimu ngazi ya Maandalizi (ECD) ambapo wanaume ni 18 na wanawake ni 207.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

31. **Mheshimiwa Spika**, huduma ya ukaguzi wa elimu inatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Lengo la huduma hii ni kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inafuata sera, sheria, miongozo na taratibu zilizopo. Kwa mwaka wa fedha

2021/22, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya TSh. 1,089,300,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 183,700,000/- ni kwa ajili ya kazi za ukaguzi wa skuli na TSh. 905,600,000/- ni malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2022, jumla ya TSh. 722,460,170/- zilipatikana sawa na asilimia 66. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya skuli 729 (538 za Serikali na 191 za binafsi) Unguja na Pemba sawa na asilimia 81 ya makadirio ya skuli zilizopangwa kukaguliwa zimekaguliwa. Kati ya skuli hizo, 79 ni za Maandalizi, 322 ni za msingi na 328 za sekondari.
- ii. Jumla ya walimu 2,048 wamekaguliwa na kupewa ushauri kulingana na masomo wanayofundisha Unguja na Pemba. Ushauri huu umezingatia mbinu za usomeshaji na matumizi ya vifaa vya kufundishia.
- iii. Mafunzo ya matumizi ya muongozo wa ukaguzi yametolewa kwa washiriki 596 wakiwemo walimu wakuu, wasaidizi walimu wakuu na viongozi wa seksheni Unguja na Pemba. Muongozo huu una lengo la kuimarisha ufanisi katika kufanya ukaguzi wa ndani wa skuli.
- iv. Upimaji wa uwezo wa wanafunzi wa darasa la pili katika kujua kusoma na kuandika umefanyika kwa wanafunzi 1,805 katika skuli 95 za Unguja na Pemba. Matokeo ya upimaji huu unaonesha kuwa asilimia 65

ya wanafunzi bado wanachangamoto ya ufahamu wa wanachokisoma pamoja na uandishi wa Imla.

Matokeo ya Muda mfupi

- i. Jumla ya skuli 729 (538 za Serikali na 191 za binafsi) Unguja na Pemba zimekaguliwa.
- ii. Jumla ya walimu 2,048 wamekaguliwa na kupewa ushauri kulingana na masomo wanayofundisha, Unguja na Pemba.
- iii. Mafunzo ya matumizi ya muongozo wa ukaguzi yametolewa kwa washiriki 596 wakiwemo walimu wakuu, wasaidizi walimu wakuu na viongozi wa seksheni Unguja na Pemba.
- iv. Maandalizi ya miongozo ya viwango vya majengo pamoja na viwango vya walimu imeandaliwa na iko katika hatua za mwisho cha uchapaji.

Huduma za Maktaba

- 32. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na watu wote. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku yenye jumla ya TSh. 1,027,900,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 573,100,000/- ni kwa ajili ya kuimarisha huduma za maktaba na TSh. 454,800,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2022, Jumla ya TSh. 422,372,760/- sawa

na asilimia 41 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya watumiaji 24,353 walifika maktaba kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali ikiwemo uazimaji na usomaji vitabu na kutafuta taarifa za kitaaluma.
- ii. Jumla ya vitabu 9,320 vya aina mbalimbali viliazimwa na kutumiwa ndani na nje ya maktaba.
- iii. Jumla ya programu 78 za watoto zimefanyika ndani ya maktaba na kuwashirikisha watoto 4,978. Lengo la programu hizo ni kuwahamasisha watoto kujenga utamaduni kupenda kusoma.
- iv. Jumla ya wanachama 1,612 wameendelea kutumia huduma za intaneti katika maktaba zetu Unguja na Pemba.
- v. Jumla ya nakala 2,661 za magazeti zimenunuliwa na kuingizwa Maktaba ili kuwapa fursa wananchi kupata tarifa za matokeo mbalimbali ya kila siku. Magazeti hayo ni Zanzibar leo, Nipashe, Habari leo, Uhuru, Mzalendo, Guardian, East African na Daily News.
- vi. Maktaba kuu ya tawi la Dunga Wilaya ya Kati Unguja imeanzishwa pamoja na maktaba za skuli kwa skuli mbili (kijichi na Kizimbani) Unguja na Pemba. Aidha, uimarishaji wa maktaba kwa skuli za Pete, Kilombero, Pongwe Pwani, Jadida na Miti Ulaya umefanyika.
- vii. Jumla ya wafanyakazi saba wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali Tanzania. Kati yao sita katika

ngazi ya Shahada fani ya Ukutubi na mmoja katika ngazi za stahhada katika chuo Kikuu huria Tanzania.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Jumla ya wanachama wapya 367 (316 watu wazima na 51 watoto) walisajiliwa katika Maktaba za Bodi.
- ii. Idadi ya watumiaji wa maktaba imefikia 27,186. Miongoni mwao 9,531 ni wanawake, wanaume ni 10,256 na 7,402 ni watoto.

Huduma ya Urajisi wa Elimu

33. Mheshimiwa Spika, Huduma hii inamadhuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa katika skuli za Serikali na Binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na Binafsi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku yenye jumla ya TSh. 258,900,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 121,200,000/- ni kwa ajili ya shughuli za urajisi na utoaji wa leseni na TSh. 137,700,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2022, Jumla ya TSh. 151,311,545/- sawa na asilimia 58 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Ufuatiliaji wa wanafunzi waliopata ujauzito kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 unaendelea ambapo jumla ya wanafunzi 96

(Mkoa wa Kaskazini Unguja 47 na Wilaya ya Wete 49) waligundulika kuwa na ujauzito. Jumla ya kesi 32 (15 Unguja na 17 Pemba) za ujauzito zimeripotiwa katika Ofisi ya Mrajisi wa Elimu na kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa husika. Kati ya kesi hizo, kesi 12 zimejadiliwa na ofisi ya Mrajis wa Elimu Unguja na 10 zimejadiliwa ofisi ya Naibu Mrajis Pemba kwa mujibu wa Sheria namba 4 (2005) ya kuwalinda Wari na Mtoto wa Mzazi Mmoja ambayo imewapa fursa wanafunzi hawa kuendelea na masomo yao.

- ii. Ufuatiliaji wa wanafunzi waliodhalilishwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 unaendelea ambapo Jumla ya wanafunzi 63 (20 Unguja na 43 Pemba) wamefuatiliwa. Jumla ya kesi 25 za udhalilishaji (2 Unguja na 23 Pemba) zikiwemo ubakaji na ulawiti zimeripotiwa katika Ofisi za Mrajisi. Aidha, Kesi moja ya ndoa ya mwanafunzi imeripotiwa katika Ofisi ya Naibu Mrajis Pemba. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 6 ya mwaka 1982 kifungu cha 20(3) kwamba mwanafunzi huyo haruhusiwi kuendelea na masomo yake.
- iii. Zoezi la utoaji wa leseni mpya za walimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki linaendelea kwa walimu wa Sekondari wa Wilaya ya Mkoani Pemba na taarifa zao zimeshaingizwa katika kompyuta na kupigwa picha. Aidha, jumla ya walimu 408 (255 wanaume na 153 wanawake) wameshapatiwa leseni zao za kielektroniki.

- iv. Jumla ya walimu 2,170 wakiwemo wa Cheti cha Ualimu, Stashahada, Shahada ya Kwanza na ya Pili walipatiwa leseni za kufundishia za muda wa miaka mitano. Aidha, Walimu 425 ambao hawajasomea wamepatiwa leseni za kufundishia za muda wa mwaka mmoja. Walimu hawa wanatakiwa kuomba vyyuo mbalimbali ili kupewa mafunzo ya ualimu.
- v. Jumla ya skuli 5 za Serikali zimepatiwa usajili zikiwemo skuli 1 ya maandalizi na msingi, 3 za msingi na 1 ya sekondari kwa Unguja na Pemba.
- vi. Jumla ya skuli 34 za binafsi zimewasilisha maombi ya usajili wa muda. Kati ya hizo, 18 za maandalizi, 14 za maandalizi na msingi, skuli 1 ya maandalizi msingi na sekondari na skuli 1 ya sekondari.
- vii. Jumla ya vyyuo viwili vimewasilisha maombi ya usajili wa fani ya ualimu vikiwemo Chuo cha Singida Teacher College kilichopo Wingwi Pemba na chuo cha Teacher Centre kilichopo Kwamchina Unguja. Chuo cha Singida Teacher College kimepatiwa usajili kutoa mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya cheti na diploma.
- viii. Jumla ya skuli 527 za ngazi mbalimbali za serikali na binafsi zimehakikiwa.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya skuli 5 za Serikali zimepatiwa usajili zikiwemo skuli 1 ya maandalizi na msingi, 3 za msingi na 1 ya sekondari kwa Unguja na Pemba.

- ii. Skuli 11 kati ya 34 zilizowasilisha maombi ya usajili wa muda zimepewa usajili wao baada ya kukaguliwa. Skuli ambazo hazijasajiliwa zinaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi ili kupatiwa usajili husika.
- iii. Jumla ya skuli 34 za binafsi zimewasilisha maombi ya usajili wa muda. Kati ya hizo, 18 za maandalizi, 14 za maandalizi na msingi, skuli 1 ya maandalizi msingi na sekondari na skuli 1 ya sekondari. Skuli 11 zimepewa usajili wao baada ya kukaguliwa.
- iv. Chuo cha Singida Teacher College kimepatiwa usajili kutoa mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya cheti na diploma.
- v. Jumla ya skuli 527 za ngazi mbalimbali za serikali na binafsi zimehakikiwa.

Programu Ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

- 34. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama wa taarifa. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh.592,834,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 284,705,000/- ni kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika elimu na TSh. 308,129,000/- ni kwa

malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 312,632,775/- zilipatikana sawa na asilimia 52.7. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Wizara imeandaa vipindi 60 vya redio vya stadi za Maisha kwa ajili ya kuelimisha wanafunzi na changamoto mbalimbali zinazowapelekea kuacha masomo.
- ii. Watendaji 31 wa Kituo cha Habari katika Elimu (KMEC) wamepatiwa mafunzo ya kutengeneza na kurusha vipindi vya redio na TV vya kijamii na kielimu kufuatia uzinduzi wa TV na REDIO za Elimu.
- iii. Uimarishaji wa miundo mbinu ya TEHAMA katika taasisi mbali mbali zilizo chini ya WEMA ikiwa ni pamoja na kuunganisha Network katika ofisi mbali mbali zilizopo katika Makao Makuu ya Wizara Unguja na Pemba.
- iv. Wizara imeimarisha mifumo mbali mbali ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na mfumo wa tathmini za wanafunzi. Mfumo huu humuwezesha mwalimu, mzazi na mwanafunzi kupata taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kwa urahisi. Pia mfumo wa kuwapangia skuli wanafunzi wanaoingia Kidato cha Tano kulingana na Tahasusi zao za masomo pamoja na mfumo wa kujipima uwezo wa kujibu mitihani kwa wanafunzi.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Uwepo wa mfumo wa upatikakanaji wa taarifa za maendeleo ya wanafunzi katika masomo yao kwa wazazi.

Programu Ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

35. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2021/22 programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 100,000,000/- kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2022, jumla ya TSh. 19,075,885/- sawa na asilimia 19 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya washiriki 65 wakiwemo walimu 12 na wanafunzi 53 (20 wanaume 33 na wanawake) wenye uziwi pamoja na marafiki zao wanaowasaidia katika masomo walipatiwa mafunzo ya lugha ya alama.
- ii. Jumla ya walimu 1,213 (326 wanaume na wanawake 887) kutoka Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo ya stadi za Maisha ili kuwasaidia wanafunzi waweze kujiamini na kuwa na uthubutu wa kupambana na changamoto za udhalilishaji zinazopelekea kuharibu ujifunzaji wao
- iii. Kazi ya kukusanya taarifa za wanafunzi wenye ulemavu ili kujua idadi yao na skuli wanazosoma imefanyika katika skuli 216 (166 za Unguja na 50 za Pemba) na

kugundua kuwa kuna wanafunzi 50 wasioona kabisa, 634 wenye uoni hafifu, 197 viziwi, 231 usikivu mdogo, 512 ulemavu wa akili, 339 ulemavu wa viungo na 15 wenye ualbino.

- iv. Ziara za ufuatiliaji katika skuli 120 (Unguja 70 na Pemba 50) zimefanyika kwa lengo la kuona njia zinazotumika katika kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- v. Vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu vikiwemo Shimesikio 200, fimbonyeupe 65, mashine za kuandikia nukta nundu 40, virekodi sauti 40, kompyuta laptop 10, 'telescope' 17, miwani 2,319, lenzi za mkononi za kukuzia maandishi 14, viti vya magurudumu matatu 10, viti vya magurudumu mawili 48, 'Kid walk' 4, mikono na miguu bandia 117 vimenunuliwa na kusambazwa kwa wanafunzi wenyemahitaji maalum Unguja na Pemba.
- vi. Jumla ya wanafunzi 1,220 (540 wanume na wanawake 680) kutoka skuli 20, wamepatiwa mafunzo ya namna yakujjepusha na mimba za umri mdogo na ndoa za mapema.
Matokeo ya muda mfupi;
- i. Skuli zilizopatiwa mafunzo ya stadi za maisha zimeongezeka kutoka 40 mwaka 2021 hadi 78 mwaka 2022.

Programu Ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Elimu

36. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 742,863,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 534,705,000/- ni kwa kuendesha shughuli za michezo na utamaduni na TSh. 208,158,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 309,099,590/- sawa na asilimia 42 zilipatikana. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya walimu 25 walipatiwa mafunzo ya uamuzi wa mchezo wa Netiboli. Walimu 30 walipatiwa mafunzo ya michezo kwa watoto kupitia mradi wa Coaching Across Continent kwa mashirikiano na Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu.
- ii. Jumla ya wafanyakazi 35 (25 Unguja na 10 Pemba) wamejengewa uwezo juu ya Ubunifu katika kazi
- iii. Walimu 11 walipatiwa mafunzo ya walimu wa walimu wa kufundisha kuogelea (Master trainers) Unguja na Pemba.
- iv. Walimu 88 na wanafunzi 550 katika Skuli za Msingi na Sekondari walipatiwa mafunzo ya kuogelea. Aidha, Walimu 300 walipatiwa mafunzo ya usalama na uokozi kwenye maji Unguja na Pemba kwa kushirikiana na Taasisi ya The Panje Project.

- v. Mafunzo ya awali kwa walimu 45 wa Mpira wa Mikono (Handball) yalitolewa kwa kushirikiana na Jumuiya ya ZESI na mtaalamu kutoka Sweden.
- vi. Jumla ya wanafunzi 368 (Wanaume 200 na wanawake 168) wa skuli za Msingi na Sekondari walishiriki katika mashindano ya Mbio za Nyika (Elimu Cross Country). Miongoni mwa wanafunzi hao watashiriki katika mashindano ya Michezo ya Kitaifa yakiwemo UMITASHUMTA kwa Skuli za Msingi na UMISSETA kwa Skuli za Sekondari.
- vii. Jumla ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari 189 wa Zanzibar walishiriki katika mashindano ya UMISSETA yaliyofanyika huko Mtwara Tanzania Bara na kufanikiwa kupata ubingwa wa michezo 6 ikiwemo Mpira wa Miguu, Mpira wa Mikono (Handball), Mpira wa Meza, Riadha, Mpira wa Wavu na Mpira wa Kikapu.
- viii. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeadhimisha Tamasha la miaka 57 ya Elimu bila Malipo lililofanyika tarehe 23/09/2021 uwanja wa Gombani Pemba. Maadhimisho hayo yalijumuisha mashindano ya michezo na sanaa kuanzia ngazi ya Skuli, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.
- ix. Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali ilishiriki katika mashindano ya wanafunzi wa skuli za Sekondari (Mapinduzi Cup) kwa mchezo wa Netiboli kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ambapo jumla ya skuli 15 kutoka Wilaya za Unguja zilishiriki. Aidha, Timu ya wafanyakazi wa Wizara walishiriki

katika mashindano ya Mapinduzi Cup kwa mchezo wa Mpira wa Miguu na Netiboli, ambapo timu ya mpira wa miguu imeibuka bingwa wa michuano hiyo.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Kufanikiwa kupata ubingwa wa michezo 6 ikiwemo Mpira wa Miguu, Mpira wa Mikono (Handball), Mpira wa Meza, Riadha, Mpira wa Wavu na Mpira wa Kikapu katika mashindano ya UMISSETA.
- ii. Jumla ya walimu 25 walipatiwa mafunzo ya uamuzi wa mchezo wa Netiboli.
- iii. Walimu 11 walipatiwa mafunzo ya walimu wa walimu wa kufundisha kuogelea (Master trainers) Unguja na Pemba.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

- 37. Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu ya Utawala na Uongozi ni kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali bora na usimamizi mzuri wa matumizi yake katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa ujumla, programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za elimu Pemba.

Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla

- 38. Mheshimiwa Spika,** programu ya Uongozi ina lengo la kuhakikisha ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya

Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, programu hii ilipangiwa jumla ya TSh. 6,978,782,000. Kati ya fedha hizo, TSh. 3,411,121,000/- ni kwa ajili utekelezaji wa shughuli za utumishi na uendeshaji na TSh. 3,567,661,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh. 3,950,739,454/= zilipatikana sawa na asilimia 57. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Wizara imefanya uhakiki wa mahitaji ya walimu wanaohitajika kwa ngazi zote za elimu. Taarifa ya uhakiki huo zimewasilishwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya hatua zinazofuata za uajiri wa walimu. Uhakiki huo umeonesha kuwa jumla ya walimu wapya 816 wa masomo ya sayansi wanahitajika kwa Unguja na Pemba wakiwemo walimu 259 wa Fizikia, 74 wa Kemia, 53 wa Biolojia na walimu 430 wa Hisabati.
- ii. Idara inaendelea na kusimamia na kutoa huduma kwa wafanyakazi wote 16,407 wakiwemo wafanyakazi 10,752 wanawake na 5,655 wanaume. Wafanyakazi 12,177 wapo Unguja na 4,230 wapo Pemba. Kati ya wafanyakazi hawa wote walimu ni 14,594 na kada nyingine 1,813.
- iii. Wizara imeendelea kuratibu mafunzo ya wafanyakazi ambapo jumla ya wafanyakazi 124 walipatiwa fursa ya kujiunga na masomo katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi katika ngazi tofauti baada ya kukamilisha masharti ya kiutumishi na ya vyuo husika.

- iv. Jumla ya wafanyakazi 2,038 waliopewa likizo walilipwa posho la likizo, jumla ya TSh 203,800,000/- zimelipwa na jumla ya wafanyakazi 591 wamelipwa malimbikizo yao ya mishahara yenye jumla ya TSh 297,653,779.
- v. Jumla ya wafanyakazi 147 walistaafu kazi kwa mujibu wa sheria, wakiwemo 101 kwa Unguja na 46 kwa Pemba. Pia wafanyakazi 15 waliacha kazi kwa sababu mbalimbali, wafanyakazi 40 walipewa uhamisho kwenda kuendelea na kazi katika Wizara na Taasisi mbali mbali, wafanyakazi 13 wamechukua likizo bila ya malipo na wafanyakazi 26 wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amiin.
- vi. Wizara imewadhamini jumla ya wafanyakazi 395 Unguja na 249 Pemba kupata mikopo ya Benki na Taasisi nyengine za kifedha ili kuwawezesha kutatua changamoto zao zikiwemo za vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Wafanyakazi hawa wote walifaidika na mikopo yenye thamani ya TSh. 2,234,286,378/- kwa Unguja na TSh. 51,172,427/- Pemba.

Matokeo ya muda mfupi;

Hadi kufikia Aprili 2022, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 16,407 (5,655 ni wanaume na 10,752 wanawake). Wafanyakazi 12,177 wapo Unguja na 4,230 wapo Pemba. Kati ya wafanyakazi hawa wote walimu ni 14,594 na kada nyingine 1,813

Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

39. Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina jukumu la kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilipangiwa kutumia jumla ya TSh 7,845,088,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 4,151,546,000/- ni kwa ajili ya kazi za maendeleo na TSh. TSh. 3,693,542,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikiwemo TSh. 638,337,000/- za malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2022 jumla ya TSh. 1,007,476,930/- sawa na asilimia 13 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i. Uandishi wa rasimu ya Sera mpya ya Elimu umekamilika.
- ii. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Elimu umeendelea kwa kila robo mwaka na ripoti za utekelezaji zimetayarishwa. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya elimu iliyokamilika na inayoendelea. Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari (ZISP), Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi na Mradi kuimarisha Miundombinu ya Elimu kupitia fedha za IMF/COVID 19. Matokeo ya ufuatiliaji huu unaonesha kwamba Mradi wa ZISP upo katika hatua za kukamilika ambapo Vituo vya Ubunifu vinaendelea kutoa huduma kwa walimu na wanafunzi, fedha za ruzuku za skuli kujiendesha

zinaendelea kutolewa, walimu wamepatiwa mafunzo yaliyopelekea kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi wao na kuongeza ufaulu. Aidha, Mradi wa Uimarishaji Miundombinu ya Elimu kupitia fedha za IMF/COVID 19 upo hatua nzuri baadhi ya madarasa yamekamilika yakiwemo madarasa ya skuli za Unguja Ukuu, Mbuyu maji, Kihinani, Maziwani na Ng'ombeni.

- iii. Mkutano mkuu wa tano wa mwaka wa tathmini ya elimu umefanyika. Mkutano huo uliwashirikisha wadau 150 wa elimu wa ndani na nje ya Zanzibar wakiwemo wahisani, wazazi wa wanafunzi, Wajumbe wa Kamati za skuli, Taasisi za Serikali na za watu binafsi. Mada kuu ya mkutano ilikuwa ni “Kuongeza kasi ya uwajibikaji wa walimu katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji uliobora”.
- iv. Wizara imefanya tathmini ya Mpango Mkuu wa Elimu (ZEDP II) na ripoti imeshaandaliwa. Tathmini hiyo imeonesha kwamba Mpango umetekelezwa kwa asilimia 80 mpaka kufikia mwaka 2021.
- v. Maandalizi ya Mpango Mkuu wa Elimu wa miaka mitano 2022 – 2027 yanaendelea ambapo mshauri elekezi amepatikana kwa kuanza kazi ya uchambuzi yakinifu wa sekta.
- vi. Maandalizi ya Mradi mpya wa uimarishaji wa elimu ya msingi kupitia ufadhili wa Serikali ya Sweden Chini ya Shirika la Sida yamekamilika. Utekelezaji wa mradi huo umeshaanza na utakuwa ni wa miaka mitano (2021 - 2026) utakaogharimu jumla ya US\$ 5.4 milioni.

- vii. Wizara imefanya vikao mbalimbali na wahisani wakiwemo Benki ya Dunia, AfDB, na OPEC Fund. Lengo la vikao hivyo ni kukamilisha matayarisho ya miradi mipya ikiwemo;
 - a) Mradi wa kuwajengea uwezo vijana katika soko la ajira ya uchumi wa buluu (SEBEP) utaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mradi huu unatarajiwa kuimarisha miundombinu ya Mafunzo ya Amali kwa kujenga vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali; vitatu Unguja na viwili Pemba; ujenzi wa Chuo cha Ubaharia katika eneo la SUZA kampasi ya Nkrumah; utanuzi wa jengo la karakana ya makenika katika eneo la KIST pamoja na ujenzi wa Incubator katika eneo la SUZA Kizimbani. Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya USD 50 milioni.
 - b) Mradi wa kuimarisha mafunzo ya ufundi kwa kujenga Skuli za Sekondari za Ufundi 11 Unguja na Pemba kupitia ufadhili wa OPEC Fund. Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya USD 60 milioni.
 - c) Mradi wa Benki ya Dunia wenye lengo la kuimarisha ubora wa elimu kwa kuimarisha miundombinu ya skuli za msingi na kusaidia utekelezaji wa mitaala mipya (ikiwemo kuwapatia walimu mafunzo pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia). Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya USD 50 milioni.
- viii. Mafunzo ya kuzisaidia skuli za Sekondari za Serikali kuandaa mipango kazi ya maendeleo ya skuli

yamefanyika kwa skuli zote za Sekondari za Serikali Unguja na Pemba.

- ix. Matayarisho ya utafiti wa kutathmini maendeleo ya wanafunzi wa elimu ya msingi (Darasa la 1 – IV) wenye lengo la kujua uwezo wa watoto katika Kuandika, Kusoma na Kuhesabu yanaendelea, ambapo kazi ya andiko la dhana ya utafiti (Research Proposal) na matayarisho ya zana za kukusanyia taarifa imekamilika.
- x. Matayarisho ya Kitabu cha Takwimu za Elimu (Annual Statistical Abstract 2022) yanaendelea katika hatua za uchambuzi wa taarifa.

Matokeo ya muda mfupi;

- i) Skuli zote za Sekondari za Serikali Unguja na Pemba zimepatiwa mafunzo ya kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Skuli zao.
- ii) Mashirikiano kati ya Wizara na Wahisani mbalimbali wa ndani na nje katika maendeleo ya elimu yameimarika.
- iii) Uwepo wa taarifa za elimu katika ngazi zote zinazosaidia kufanya maamuzi sahihi.

Programu Ndogo ya Uratibu shughuli za Elimu Pemba

40. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya TSh. 3,546,762,000/-. Kati ya

fedha hizo, TSh. 511,305,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 3,035,457,000/- ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2022, jumla ya TSh.2,761,689,969/- zilipatikana sawa na asilimia 78. Fedha za programu hii zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli zote na programu za elimu Pemba.

MAPATO

- 41. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukusanya mapato kupitia usajili wa Skuli za binafsi na malipo ya leseni za walimu. Hadi kufikia Aprili 2022, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya TSh.225,572,008/- kati ya TSh. 283,170,000/- zilizopangwa kukusanywa. Hii ni sawa ya asilimia 80 ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanywa TSh. 109,459,950/- zinatokana na malipo ya leseni za walimu na TSh. 116,112,058/- ni za usajili wa skuli za binafsi.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2022/2023 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU

- 42. Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22 naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kuzingatia vipaumbele vya Wizara.

Vipaumbele vya Wizara

- i. Kuandaa Mpango wa miaka mitano wa Maendeleo ya Elimu (2022/23 – 2026/27)
- ii. Uajiri wa walimu 4227 wapya kukidhi mahitaji ya walimu Unguja na Pemba katika ngazi zote za elimu zikiwemo mafunzo ya amali na ufundi.
- iii. Kuzipatia Ruzuku ya Fedha Skuli zote za Serikali kwa ajili ya gharama za uendeshaji.
- iv. Kukamilisha uandishi wa Mihutasari ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, kuandika vitabu pamoja na kuwapatia mafunzo walimu wote wa maandalizi na msingi kufuatia kukamilika kwa mitaala mipya ya elimu ya ngazi hizo.
- v. Kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga skuli mpya 12, kujenga madarasa mapya 50 na kukamilisha madarasa 50 yaliyoanzishwa kwa nguvu za Wananchi. Skuli zitakazojengwa ni; mbili za maandalizi, mbili za msingi, na nane za Sekondari zikiwemo skuli tatu zenye dahalia na Skuli ya Sekondari ya Ufundi, Aidha, Skuli za Sekondari za Ufundi za Kengeja na Mikunguni zitafanyiwa ukarabati mkubwa na skuli tano za msingi zitafanyiwa ukarabati mdogo.
- vi. Kujenga karakana za Elimu ya Amali kwa ajili wa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika skuli za elimu mjumuisho Jendele na Pujini pamoja na kuzipatia vifaa vya elimu ya Ufundi.
- vii. Kuendelea na programu ya lishe katika skuli za msingi 42 zilizo katika mazingira magumu.

- viii. Kutoa mafunzo kwa walimu wa Sekondari kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza pamoja na kuimarisha mazingira rafiki ya kujifunza na kufundishia katika skuli kwa kuzipatia skuli vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum.
 - ix. Kujenga maabara katika skuli 10 za Sekondari kwa lengo la kuimarisha Elimu ya Sayansi kwa wanafunzi wa Sekondari Unguja na Pemba pamoja na kuimarisha mifumo ya Teknolojia katika Skuli, Vituo vya Walimu na Vituo vya Ubunifu.
 - x. Kujenga Vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali katika maeneo ya Fumba, Jendele, Mangapwani, Tumbe na Chambani pamoja na Chuo cha ubaharia katika eneo la SUZA Kampasi ya Nkrumah pamoja na kuvipatia vyuo vya Amali vifaa vya kisasa ili viweze kutoa mafunzo ya vitendo na nadharia.
 - xi. Kuimarisha huduma ya Ukaguzi wa skuli, huduma za maktaba pamoja na kuzipatia skuli vifaa vya michezo.
 - xii. Kuendelea kutoa Mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu.
- 43. Mheshimiwa Spika**, Sasa naomba kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo:
- 44. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza

malengo yake yaliyozingatia malengo ya Taifa ya Dira 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya elimu nchini. Wizara pia itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mitatu ya maendeleo ya elimu ambayo ni:-

- i. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi
- ii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
- iii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali

MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU

45. **Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria, Shabaha za utekelezaji kwa kila programu na jumla ya gharama za matumizi zilizopangwa kutumika kwa kila programu.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

46. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu ya sekondari.

Matokeo ya muda mfupi;

- Wanafunzi waweze kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Viashiria vya matokeo;

- Asilimia ya uandikishaji.
- Uwiano wa idadi ya walimu kwa wanafunzi.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi.

Shabaha za utekelezaji;

- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi wa msingi kutoka asilimia 70.0 kwa mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2023.

Gharama za Programu:

Jumla ya TSh. 91,562,332,000/- zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 70,602,619,000/- ni kwa kazi za kawaida na TSh. 20,959,713,000/- kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

- 47. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuongezeka uandikishaji na ufaulu wa wanafunzi wa elimu ya Sekondari katika mitihani ya taifa.

Viashiria vya matokeo;

- Asilimia ya uandikishaji
- Asilimia ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya lazima,
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi na wanaoendelea katika ngazi ya kidato cha nne, cha sita na elimu ya juu.
- Uwiano wa idadi ya wanafunzi na walimu.
- Uwiano wa wanafunzi kwa madarasa.

Shabaha za utekelezaji;

- Kuongezeka kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa sekondari ya awali (Kidato cha 1 – 4) kutoka asilimia 61.3 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 65.6 mwaka 2023.

Gharama za Programu:

Jumla ya TSh. 114,043,865,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya hizo TSh. 70,527,705,000/- kwa kazi za kawaida na TSh. 43,516,160,000/- kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

48. **Mheshimiwa Spika**, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujijiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo madogo manne ambayo ni: -

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

49. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Uwepo wa walimu wenye umahiri watakaokuza ubora wa elimu itolewayo

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi waliohitimu mafunzo ya ualimu.
- Idadi ya programu za mafunzo ya ualimu.

Shabaha za Utekelezaji;

- Uwepo wa mpango wa mafunzo kazini
- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka 99.3 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2023.
- Kuongeza Idadi ya programu za mafunzo ya ualimu vyaoni kutoka 6 mwaka 2021 hadi 10 mwaka 2022

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

50. **Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

Matokeo ya muda mfupi;

- Ongezeko la wahitimu wa kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu katika fani mbalimbali zinazohitajika kwa maendeleo ya nchi.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Astashahada na Stashahada.
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Shahada ya kwanza ya Uzamili na Uzamivu.
- Idadi ya tafiti zinazofanywa.

Shabaha za Utekelezaji;

Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu kutoka 9,370 mwaka 2022 hadi kufikia 9,882 mwaka 2023.

Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia

51. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia.

Matokeo ya muda mfupi;

- Uongezeko la wahitimu katika fani ya Ufundi, Sayansi na Teknolojia

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wahitimu wa fani za ufundi, Sayansi na Teknolojia,

Shabaha ya Utekelezaji

- Kuongeza wahitimu wa fani za ufundi, sayansi na

teknolojia kutoka 758 mwaka 2022 na kufikia 805 mwaka 2023.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

52. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Juu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Ongezeko la wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu.
- Ongezeko la wanafunzi wanaorejsha mikopo ya elimu ya juu.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaopokea mikopo
- Idadi ya wanafunzi wanaorudisha mikopo.

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuendelea kuwapatia mikopo wanafunzi 3,020 wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu katika vyuo mbalimbali na kuwapatia mikopo wanafunzi 1,265 wapya wataojiunga na masomo ya elimu ya juu kwa mwaka 2022/2023.
- Kuongeza makusanyo ya marejesho ya mikopo kutoka TSh. 4.2 bilioni mwaka 2021/22 na kufikia TSh. 5.0 bilioni mwaka 2022/2023.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

53. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya usimamizi na tathmini ya elimu ya juu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuimarika kwa mahusiano na mashirikiano mazuri ya uendeshaji wa Taasisi za elimu ya juu.
- Ongezeko la nafasi za wanafunzi wanaopata udhamini wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu kuongezeka.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu kijinsia.
- Idadi ya wahitimu wa elimu ya juu kijinsia.
- Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu

Gharama za Programu:

Jumla ya TSh. 31,807,492,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu kwa matumizi ya kawaida.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

54. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo mbili kama ifuatavyo;

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

55. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umasikini.

Matokeo ya muda mfupi;

- Ongezeko la wahitimu waliopata mafunzo ya amali na ufundi na kuweza kujiajiri

Viashiria vya matokeo;

- Idada ya vikundi vya wahitimu wa Mafunzo ya Amali waliopatiwa Mkopo
- Idadi ya wahitimu wa Mafunzo ya Amali

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

56. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kupunguza kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii.

Matokeo ya muda mfupi;

- Ongezeko la vijana waliorejea masomo baada ya kuacha skuli
- Ongezeko la watu waliojiunga na madasara ya wanakisomo.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya vijana wanaojiunga na madarasa ya elimu mbadala,
- Idadi ya watu wazima wanaojiunga katika madarasa ya wanakisomo,

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika kutoka asilimia 87.4 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 88.1 ifikapo mwaka 2023.

Gharama za Programu:

Jumla ya TSh. 44,071,035,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo TSh. 10,821,035,000/-ni kwa matumizi ya kawaida na TSh. 33,250,000,000/- kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

57. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu na programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo;

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

58. **Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Uwemo wa Mitaala ya Elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote za elimu

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya Mitaala
- uwiano wa wanafunzi kwa kitabu

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

59. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Upimaji wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa .

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi na walimu waliofanya mitihani
- Asilimia ya ufaulu wa walimu na wanafunzi
Shabaha za Utekelezaji
- Kuongezeka Asilimia ya wanafunzi walioandikishwa kufanya mitihani ya kidato cha pili kutoka asilimia 97.0 Mwaka 2021 na kufikia asilimia 100 mwaka 2022.
- Kiwango cha ufaulu cha mpito kutoka kidato cha pili kwenda cha tatu kuongezeka kutoka asilimia 78.7 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 85.3 ifikapo mwaka 2022.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

- 60. Mheshimiwa Spika,** utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa.

Matokeo ya Muda Mfupi

- Ongezeko la Skuli na Walimu waliofanyiwa ukaguzi

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya skuli na walimu waliofanyiwa ukaguzi

Shabaha za utekelezaji

- Kuongeza idadi ya skuli zilizokaguliwa kutoka skuli 900 mwaka 2021/2022 na kufikia skuli 938 mwaka 2022/2023.

- Kuongeza idadi ya walimu waliokaguliwa kutoka walimu 2,709 mwaka 2021/2022 na kufikia walimu 2,800 mwaka 2022/2023.

Huduma za Maktaba

- 61. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

Matokeo ya muda mfupi;

- Ongezeko la wanafunzi, vijana na wanajamii wanaopaiwa huduma za maktaba
- Ongezeko kwa vifaa vya kujisomea katika maktaba
- Ongezeko la skuli zenye huduma za maktaba kwa wanafunzi

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya watu wanaotumia maktaba
- Idadi ya vitabu, CDs, magazeti na majarida yaliyopo katika maktaba.
- Idadi ya skuli zenye maktaba kamili.

Huduma ya Urajisi wa Elimu

- 62. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa. Pia kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

Matokeo ya muda mfupi;

- Skuli za Serikali na binafsi zenye viwango bora kusajiliwa
- Leseni za walimu kutolewa.
- Kuondoa matukio ya udhalilishaji kwa wanafunzi

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya leseni za walimu zilizotolewa.
- Idadi ya skuli zilizosajiliwa.
- Sheria ya Elimu iliyopitiwa na kurekebishwa.
- Idadi ya kesi za ndoa kwa wanafunzi zilizofuatiliwa na kutolewa uamuzi.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuanza kutumia sheria ya elimu iliyofanyiwa mapitio

Programu Ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

- 63. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuimarika kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- Idadi ya Skuli zenye mazingira yaliyozingatia mahitaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum

Shabaha ya Utekelezaji

- Kujenga skuli mbili maalum za elimu mjumuisho

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

64. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika kujifunza, kufundisha, ngazi ya utawala na katika maisha ya kila siku.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA kwa walimu na wanafunzi katika kujifunza na kufundishia.

Viashiria vya utekelezaji;

- Idadi ya walimu wenye ujuzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano,
- Idadi ya Skuli zenye vifaa vya Teknolojia ya Habari na mawasiliano
- Idadi ya vipindi vya masomo vitakavyorushwa hewani kupitia Redio na TV ya Elimu

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya walimu wenye ujuzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kutoka walimu 250 hadi kufikia walimu 500.
- Kuongeza idadi ya Vipindi vya masomo katika Redio na TV za Kituo cha Habari cha Mawasiliano Kwarara (KMEC) kutoka 60 na kufikia 100 mwaka 2023.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli

65. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika michezo.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya walimu wenye taaluma ya michezo
- Idadi ya skuli zenye viwanja vya michezo
- Idadi ya skuli zenye vifaa vya michezo
- Idadi ya wanafunzi wenye vipaji vya michezo

Shabaha ya Utekelezaji

- Koungeza ushindani na ushiriki michezo katika ngazi za kikanda na kitaifa na kushinda vikombe zaidi kutoka 6 mwaka 2021 mpaka 12 mwaka 2022.

Gharama za Programu:

Jumla ya TSh. 11,328,250,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii kwa kazi za kawaida.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

66. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumiwa kwa kuimarisha utoaji wa elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu kama zifuatavyo: -

Programu ndogo ya Uongozi kiujumla

67. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuratibu usimamizi na ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kupatikana kwa ufanisi katika utoaji wa huduma, uongozi na utawala wa rasilimali za Wizara.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wafanyakazi wanaoajiriwa na kustaafu,
- Idadi ya wafanyakazi waliopatiwa mafunzo.

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza idadi wa wafanyakazi kutoka 16,407 mwaka 2022 na kufikia 20,634 mwaka 2023 wakiwemo walimu.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti

68. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kufanikisha na kuratibu Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara.

Matokeo ya muda mfupi;

- Uwepo wa Sera na Mipango inayozingatia mahitaji ya Maendeleo ya Sekta ya elimu
- Ongezeko la miradi ya Maendeleo ya Elimu.
- Uwepo wa taarifa za upimaji wa maendeleo ya mpango ya elimu

Viashiria vya matokeo;

- Idadi za tafiti zilizofanywa
- Uwepo wa Sera mpya ya mwaka 2022
- Uwepo wa Mpango Mkuu wa Elimu

- Uwepo wa Ripoti za utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya Elimu.
- Idadi ya miradi mipya iliyoibuliwa

Shabaha ya Utekelezaji

- Kukamilisha mpango Mkuu wa Elimu 2022 – 2027 na Kuandaa mpango wa utekelezaji (Operational Plan)
- Kukamilisha Sera ya Elimu ya mwaka 2022
- Kufanya tafiti mbili za elimu
- Kukamilisha Kitabu cha takwimu za Elimu (Annual Statistical Abstract)
- Kuandaa ripoti za mafanikio ya Sekta ya Elimu
- Kukamilisha maandalizi ya Miradi Minne ya elimu
- Kuimarisha mashirikiano na wahisani waliopo na kuanzisha mashirikiano na wahisani wapya

Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba

69. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Matokeo ya muda mfupi na viashiria vya utekelezaji vinavyotumika ni kama vile vilivyoielezwa katika programu za uongozi kiujumla na uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti.

Gharama za Programu:

Jumla ya TSh. 17,002,098,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

MAKADIRIO YA MAPATO

- 70. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakadiria kukusanya jumla ya TSh. 396,396,000/- ikiwa ni mapato kutoka katika vyanzo vyake vikuu ambavyo ni leseni za walimu, ada ya usajili wa skuli za binafsi na ada ya usajili ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano wanaotoka katika skuli za binafsi

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

- 71. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TSh. 309,815,073,000/= zitahitajika katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya sekta ya Elimu. Kati ya hizo TSh. 249,063,699,000 /= ni za SMZ na TSh. 60,751,374,000/= ni kutoka kwa Wahisani. Fedha zinazotoka SMZ, TSh. 36,974,499,000/= ni za miradi ya Maendeleo, TSh.149,986,400,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na TSh 62,102,800,000/= ni kwa matumizi ya kawaida. Aidha, fedha kutoka kwa wahisani TSh. 18,546,374,000/= ni za ruzuku kwa miradi ya maendeleo kutoka GPE, UNICEF, KOICA, Table for Two (TfT), Shirika la Good Neighbors la Korea na Milele Zanzibar Foundation na TZS. 40,085,000,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA). Kati ya fedha zote TSh. 97,725,873,000 sawa na asilimia 31.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na TSh. 212,089,200,000/-

sawa na asilimia 68.5 ni matumizi ya kawaida zikijumuisha mishahara ya wafanyakazi.

SHUKURANI

- 72. Mheshimiwa Spika,** nachukuwa fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wote wa maendeleo ya elimu wa ndani na nje waliotuunga mkono na kutoa mashirikiano katika utekelezaji wa mpango wa sekta ya elimu. Miongoni mwa washirika hao ni wanafunzi wenyewe, wazazi, washirika wa maendeleo na mashirika ya misaada ya kimataifa. Tunatoa shukurani zetu za pekee kwa mashirika mbalimbali yakiwemo Sida, KOICA, USAID, UNESCO, UNICEF, VSO, GPE, Good Neighbors, na Table for Two, Kampuni ya BOPAR, AL-BAWARDY, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, IFRAJ FOUNDATION na JUMUIYA YA WAZAZI. Pia shukurani zetu za dhati kwa Aga Khan Foundation, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Napenda pia, kuyashukuru mashirika yasio ya kiserikali yakiwemo Milele Zanzibar Foundation, Jumuiya ya Madrasa Early Childhood Education Program, NFU, FAWE, Save the Children Fund, Book Aid International na ZAPDD. Vile Vile napenda kuyashukuru makampuni na mashirika mbalimbali ya kifedha kama Benki ya watu wa Zanzibar, CRDB, NBC, NMB, Postal Bank Tanzania, ZANTEL, SACCOS mbalimbali na Tigo kwa misaada yao katika sekta yetu ya elimu na kwa wafanyakazi kwa ujumla.

- 73. Mheshimiwa Spika,** Shukurani za pekee kwa Chama changu cha Mapinduzi kuanzia Taifa hadi Shina kwa kuwajali wananchi wote na kuendelea kusimamia maendeleo ya taifa letu. Aidha, shukurani kwa familia yangu kwa ushirikiano na utulivu wanaonipatia.
- 74. Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kutanguliza shukurani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu kuanzia wewe Mheshimiwa Spika kiongozi wetu na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa mnaoendelea kunipa na kwa namna mtakavyoichangia hotuba yangu hii, nasema ahsanteni sana.
- 75. Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishhe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya jumla ya TSh. 309,815,073,000/= kwa mwaka wa fedha 2022/23, ili kuiwezesha Wizara yetu hii kutekeleza majukumu yake.
- 76. Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

KIAMBATISHO

(Takwimu za Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Kwa Kipindi cha 2017/18 - 2021/22 na Hali Halisi ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2021/22)

JADWELI NAM. 1

UKUAJI WA IDADI NA AINA ZA VITUO VYA ELIMU VILIVYOSA-JILIWA, 2018 - 2022

AINA ZA VITUO	2018	2019	2020	2021	2022		JUMLA
					SERIKALI	BINAFSI	
VITUO VYA TuTu	302	342	366	390	394	0	394
SKULI ZA MAANDALIZI	347	382	363	492	41	294	335
SKULI ZA MSNGI (DAR 1- VII)	357*	381*	431*	477*	312	222	534
SKULI ZA MSNGI/KATI 'A' (DAR 1- KID 2)	38	29	17	12	10	17	27
SKULI ZA MSNGI/KATI 'B' (DAR 1- KID 4)	54	59	46	59	22	22	44
SKULI ZA MSNGI/SEKOND.(DAR 1- KID 6)	9	9	9	8	0	3	3
SKULI ZA KATI 'A' FORM 1 - FORM 2	3	7	26	24	15	9	24
SKULI ZA SEKOND. FORM 1 - FORM 4	135	136	169	169	175	39	214
SKULI ZA SEKOND. YA JUU (FORM 1 - 6)	11	26	26	29	13	9	22
SKULI ZA SEKOND. YA JUU (FORM 5 - 6)	-	-	2	1	1	1	2
SKULI ZA MCHEPUO WA KIFARANSI	1	1	0	1	1	0	1
SKULI ZA MCHEPUO WA UFUNDI	2	2	2	2	2	0	2
SKULI ZA MCHEPUO WA BASHARA	1	2	0	3	3	0	3
SKULI ZA MCHEPUO WA KISLAMU	2	2	0	2	2	0	2
SKULI ZA MCHEPUO WA SAYANSI JAMII	1	2	0	0	0	0	0
SKULI ZA MCHEPUO WA SAYANSI	7	8	0	10	7	1	8
SKULI ZA MCHEPUO WA KOMPIYUTA	1	3	0	2	1	0	1
